UTUNZAJI MAZINGIRA

Mkazi wa jiji la Dar es Salaam akitupa chupa za plastiki kwenye kifaa cha kuhifadhi takataka kilichotengenezwa kwa umbo la samaki katika ufukwe wa bahari ya Hindi eneo la Coco, jana. Kifaa hicho kimetengenezwa na Africraf ili kuhamasisha usafishaji wa mazingira kwenye maeneo ya fukwe. **Picha na Ericky Boniphace**

AFYA

MWANANCHI UK 20.

Hatari yatajwa dawa za kuua nzi mabuchani

Wataalamu wa afya waonya, wataja magonjwa yanayoweza kusababishwa na dawa hizo.

Waandishi Wetu, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

Dar/Mikoani. Matumizi ya dawa za kuulia wadudu warukao na watambaao katika mabucha ya nyama, yametajwa yanaweza kusababisha madhara ya kiafya ya muda mrefu na mfupi kwa walaji.

Dawa hizo zimetajwa kusababisha magonjwa ya figo, ini, saratani, kuvuruga mfumo wa homoni, kuathiri mfumo wa uzazi, ubongo, athari katika afya ya mjamzito na mtoto, kuharibu viungo muhimu vya mwili, kuathiri mfumo wa upumuaji na ngozi.

Hayo yameelezwa na wataalamu wa afya kutokana na kuenea taarifa ya kuwapo matumizi ya dawa mbalimbali kwa lengo la kuua nzi katika baadhi ya mabucha.

Kutokana na hali hiyo, Bodi ya nyama nchini imetoa onyo juu ya matumizi ya dawa hizo katika mabucha.

Msajili wa bodi hiyo nchini, Dk Daniel Elias Mushi alisema kitu chochote kinachotumika kuua wadudu ni hatari kwa afya kinapoingia katika mwili wa binadamu.

"Hizo dawa zimetengenezwa kwa ajili ya kuua wadudu kiasi kwamba ukimpulizia anakufa, inamaanisha dawa hizo zina sumu inayomfanya mdudu huyo kupoteza uhai," alisema.

Alisema matumizi ya dawa hizo ni hatari kwa afya ya walaji, kwani zanaweza kusababisha maradhi mbalimbali ikiwemo saratani.

Daktari Bingwa wa magonjwa ya saratani Ocean Road, Crispin Kahesa alisema dawa hizo zimetengenezwa kwa kemikali mbalimbali, hivyo zina mchango mkubwa katika kusababisha magonjwa ya saratani.

"Hizi dawa zina kemikali zinazosababisha saratani mbalimbali. Ni lazima kuangalia kemikali zilizopo mule ndani kuona zina madhara gani zikiingia kwenye chakula, kuangalia imetengenezwa na vitu gani hapo ndipo tunahusisha ugonjwa na kemikali iliyopo," alisema Dk Kahesa.

Daktari bingwa wa magonjwa ya mfumo wa chakula na ini kutoka Hospitali ya Aga Khan, Masolwa Ng'wanasai alisema matumizi ya dawa za kuulia wadudu warukao na wataambao maeneo yenye vyakula ni hatari kwa afya ya mfumo wa chakula.

Alisema dawa hizo zina madhara ya muda mrefu na madhara ya muda mfupi kulingana na aina ya mchanganyiko wa sumu zilizowekwa.

"Inategemea hiyo dawa kuna nini, mtu atapata madhara kwenye figo au kwenye ini kuna madhara ya muda mfupi na pia yapo madhara ya muda mrefu. Suala hili lipo wazi na watu wa bodi ya nyama nadhani wanawapa maelekezo hawa wauzaji, si salama kwa chakula," alisema Ng'wanasai.

Hata hivyo, takwimu kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonyesha kuna zaidi ya vifo 220,000 vitokanavyo na athari za sumu zilizoko kwenye dawa za kuulia wadudu ikiwemo viwatilifu.

Watafiti wa maradhi ya saratani wanaeleza dawa za kuulia wadudu zinachangia kwa kiasi kikubwa kusababisha seli za saratani zinapoingia mwilini, pale mtu anapokula vyakula vilivyoathiriwa na sumu za dawa za kuulia wadudu.

Baadhi ya wafanyabiashara wa bucha za nyama Manispaa ya Mpanda na jijini Dar es Salaam wamekiri kutumia dawa hizo kuua nzi huku wengine wakisema wamekuwa wakipuliza kabla ya kuingiza nyama buchani.

Mfanyabiashara wa nyama Shaban Hamis, alisema changamoto zinazojitokeza zinasababishwa na kutokuwa na elimu ya kutosha.

"Tatizo lingine linakufikia kwa sababu huelewi madhara yake mfano kutumia sumu aina ya rungu kuua nzi buchani wengi hawafahamu madhara yake," alisema.

Muuzaji wa nyama katika moja ya bucha la kisasa lililopo Mwenge, Zhakaria Nyampala alisema siri kubwa ya kuwa na bucha lisilokuwa na nzi ni kufanya usafi wa mara kwa mara pamoja na matumizi ya vifaa vya kisasa katika kukata nyama.

"Angalia hata ujenzi wa bucha lenyewe ni wa kisasa, kuna milango na madirisha ya kisasa, vioo na usafi katika kila eneo huyo nzi atatua wapi,"alisema.

Tamko la bodi ya nyama kuhusu matumizi ya dawa za kuuwa nzi buchani iliyotolewa Disemba 2, 2021 na msajili wa bodi hiyo ilitoa katazo juu ya matumizi ya dawa hizo na kuwataka wamiliki kuzingatia usafi.

Imeandikwa na Herieth Makwetta na Mariam Mbwana (Dar) Mary Clemence (Katavi)

KAULI YA OFISA MIFUGO

Ofisa mifugo mkoa wa Katavi Zediel Mhando, alisema wamebaini kuwepo upuliziaji dawa hizo mabuchani huku akilaani vikali tabia hiyo.

Aliongeza kuwa baadhi ya wafanyabiashara hao wanatumia sumu kali kuua nzi kwenye bucha zao ikiwamo dawa za mbu akidai kuwa wahusika watachukulia hatua za kisheria.

Tarura kuondoa mpango upigaji picha magari

Bakari Kiango, Mwananchi
bkiango@mwananchi.co.tz

> Lakini sasa hivi tunataka mteja hasa wale wanaogesha kwa muda mrefu kujihudumia wenyewe kwa njia ya mtandao, kama vile wanavyonunua vifurushi vya muda wa maongezi, badala ya kuonana na wakusanya ushuru. Kwa wale wanaotumia maegesho kwa muda mchache watapaswa kuhudumiwa na wakusanya ushuru."
>
> Meneja Tarura-Dar es Salaam, Godfrey Mkinga

Dar es Salaam. Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) Mkoa wa Dar es Salaam upo mbioni kuondoa mpango wa kupiga picha (scan) gari kwa siku unaofanywa na wakusanya ushuru kwa ajili ya kuliingiza gari kwenye mfumo wa malipo ya mtandao.

Tarura imefafanua kuwa hatua hiyo itawalenga zaidi wateja wanaotumia maegesho ya muda mrefu katika maeneo mbalimbali hasa mjini, ambapo hivi sasa watapaswa kulipia Sh 2,500 kwa siku baada ya taasisi hiyo kufanya maboresho ya namna ya kulipia ada ya maegesho kwa mtandao.

"Kuna wakati tumekutana na changamoto mkusanya ushuru ame-scan mtu saa 10 jioni, halafu anamuandikia bili ya siku nzima. Wakati huku kwingine amesha-scaniwa, mteja anajikuta anadaiwa Sh 5,000 au 6,500 ambayo imezidi kiwango cha siku.

"Kuna kazi kubwa ya 'kudeal' na watu, tuliwabakiza hawa (wakusanya ushuru) ili kulinda ajira zao, lakini mfumo huu mpya kwa sio rafiki kwa sababu hawarudi n fedha nyumbani," alisema Godfrey Mkinga, Meneja wa Tarura Dar es Salaam.

Mkinga alieleza hayo wakati alipozungumza na gazeti hi huku akibainisha kwa sasa Tarura imelitenga suala la ku-scan kati maeneo mawili; kwa mteja husi na kupitia kwa wakusanya ushu waliopo maeneo mbalimbali.

"Kumekuwa na malalam hasa ikiwemo mteja kufika m saa 9 alasiri na kuondoka saa lakini anapigwa Sh2,500, kiwa cha fedha cha siku nzima. K sababu mbalimbali labda m ameombwa fedha amekataa, anakomeshwa.

Mkinga aliwataka watur wa maegesho ya Tarura ku jili kupitia App ya taasisi hiy katika mfumo wa malipo ya kali kwa kuingiza namba za s za chombo chake, ili kupata h ma ya taarifa pindi wanapot maegesho.

Mkinga alisema ku mwezi ujao, wakusanya u hawatakuwa wakiweka vi tasi vya malipo baada ya giza gari la mteja husika kw mtandao badala yake itat njia ya mtandao kumjulis kukumbusha mteja kiwang chodaiwa.

Alisema kutokana na m sho mbalimbali kwa sasa hi za maegesho zitaanza k saa moja kamili hadi saa 12

Mtumiaji wa maegesho Martin alisema hatua ya ta taarifa itasaidia wa wa maegesho kuepuka wakusanya ushuru amba dhi wamekuwa wakitak gia makubaliano na wa kuwabambikizia bili kubw

Scanned with CamScanner